


# Taarifa ya Ofisi Ya Hazina

Elder. Mwita J. Machage

## SHUKRANI

Wapendwa Wajumbe wa Mkutano wa tisa, wa Halmashauri Kuu ya Conference ya South Nyanza,

Nawasalimu kwa jina la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Ni imani yangu kuwa tangu tulipotengana baada ya kikao cha mwaka 2022, Bwana amekuwa mwema kwetu na ameendelea kuwa ngome na msaada wetu wa kila siku.

Kabla ya yote, napenda kumtukuza Mungu kwa matendo yake makuu aliyotutendea, ambayo yametuwezesha kufika hapa tulipo leo—kiuchumi na kiutendaji. Kama yasemavyo Maandiko: *"Kama si Bwana aliyekuwa pamoja nasi, Israeli na aseme sasa…"* (Zaburi 124:1). Na sisi, watu wa South Nyanza Field, tuna kila sababu ya kuthibitisha ukweli huu. Ni kwa uongozi na neema ya Mungu pekee tumeweza kupitia kipindi hiki kifupi cha takriban miaka mitatu, ambacho kimejaa shughuli nyingi, changamoto, na pia mafanikio mengi ya kiutumishi. Katika yote haya, mkono wa Bwana Umetutegemeza, naye amethibitisha kuwa mwaminifu. Kwa hiyo, hatuna budi kumtukuza Mungu kwa mioyo ya dhati na uaminifu wetu wote, tukiamini kwamba kama tulivyoshuhudia uaminifu wake, naye ataendelea kutuinua kadiri tunavyoendelea kulitumainia jina lake takatifu.

Napenda kuwashukuru kwa dhati maofisa wenzangu—Mwenyekiti na Katibu—kwa ushirikiano wa karibu tuliokuwa nao katika kipindi chote tulichotumika pamoja. Kwa hakika, ni Mungu aliyejalia umoja, maelewano, na moyo wa kushirikiana katika kutekeleza majukumu yetu ya kiutumishi. Ofisi ya Hazina inamtukuza Mungu kwa ajili yenu, kwa maana mafanikio yaliyopatikana katika idara hii yametokana na mshikamano wenu, moyo wenu wa kujitolea, na utayari wenu wa kufanya kazi kwa pamoja kwa nia moja na malengo ya pamoja. Kwa niaba ya Idara ya Hazina, nasema: Asanteni sana, na Mungu aendelee kuwaongoza na kuwatumia kwa utukufu wa Jina lake.

Nawashukuru kwa namna ya pekee Wakurugenzi wote kwa uongozi wao thabiti. Vilevile, nawashukuru Wachungaji wa Mitaa pamoja na viongozi wasaidizi wa mitaa wote kwa kujitoa kwao katika huduma na kuendeleza kazi ya Mungu kwa bidii. Natoa pia shukrani zangu kwa viongozi wa taasisi zetu zote, ikiwemo shule na Hospitali, kwa mchango wao mkubwa katika kutimiza malengo ya taasisi zetu huku wakiweka mbele maadili ya Kikristo na ubora wa huduma.

Ninawashukuru timu nzima ya Wahasibu, kutoka makao makuu hadi katika taasisi zetu mbalimbali, kwa uaminifu wao na kwa kufanya kazi kwa weledi, wakimtukuza Mungu kupitia huduma yao. Napenda pia kuwapongeza na kuwashukuru Wakaguzi wa jimbo kwa juhudi zao kubwa na kwa ufuatiliaji wa karibu katika kuhakikisha kuwa utendaji wa kazi katika makanisa mahalia unazingatia viwango na miongozo ya Kanisa la Waadventista wa Sabato.


Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa maofisa wa Union ya Kaskazini mwa Tanzania (Northern Tanzania Union Field – NTUC) kwa ushauri, malezi na maelekezo yao ya thamani waliotupatia katika kipindi chote cha uongozi wetu. Tunatambua na kuthamini jinsi Bwana alivyowatumia kwa hekima katika kuendeleza kazi yake hapa South Nyanza Field. **Mungu awabariki sana.**

## UKUAJI WA CONFERENCE

Katika kipindi cha miaka mitatu (3) tangu Mkutano Mkuu wa mwaka 2022, Conference imepata mafanikio makubwa katika ukuaji wa idadi ya waumini na washiriki, kutoka 168,258 hadi kufikia 213,530 (ongezeko la 26.9%) Ukuaji huu wa haraka ulipelekea kugawanywa kwa eneo la Conference na kuanzishwa kwa Simiyu River Field. Hadi sasa, Conference yetu inahudumia jumla ya washiriki 90,094.

Kadri idadi ya waumini inavyoongezeka, ndivyo mapato ya Conference yanavyotarajiwa kuimarika. Ukuaji huu umechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa uwezo wa kifedha wa jimbo, jambo ambalo limewezesha kuendelezwa kwa kazi ya Mungu kwa ufanisi zaidi. *(Tafadhali angalia kielelezo cha mapato ya jimbo)*

Hadi kufikia mwezi Mei, mwaka 2025, South Nyanza Field ilikuwa inahudumu katika mikoa miwili ya kiutawala, yaani Mwanza na Simiyu. Wakazi wa maeneo haya wanajihusisha na shughuli mbalimbali za kibiashara, zikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara ndogondogo, viwanda vidogo na vya kati, pamoja na uchimbaji wa madini katika baadhi ya maeneo. Shughuli hizi zimekuwa mhimili mkuu wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika mikoa hii.




*Kielelezo 1: Sekta kuu za kiuchumi za mikoa ya Mwanza na Simiyu. (Vyanzo www.mwanza.go.tz na www.simiyu.go.tz)*

Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, Mkoa wa Mwanza ulichangia takriban 7.2% ya Pato la Taifa (GDP) huku Mkoa wa Simiyu ukichangia hadi 6.07% ya pato hilo. Kwa vielelezo hivi, ni wazi kwamba eneo la South Nyanza Field limekuwa ni eneo la kimkakati katika nyanja za biashara na maendeleo ya kiuchumi. Uwepo wa shughuli nyingi za uzalishaji na miundombinu ya msingi katika mikoa hii umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa uchumi wa taifa na kuleta fursa nyingi za maendeleo kwa wananchi wa maeneo husika.

Washiriki wetu wamepata fursa ya kustawi kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali za biashara, hali ambayo imewawezesha kukuza mitaji yao na kuongeza uzalishaji. Matokeo ya mafanikio haya yamewapa waumini waaminifu uwezo wa kushiriki katika ibada ya utoaji kwa kumtolea Mungu zaka na sadaka zao, kama ilivyoagizwa katika Malaki 3:10, isemayo: *"Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu; mkanijaribu kwa jambo hili, asema Bwana wa majeshi, kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka hata isiwepo nafasi ya kutosha."*



*Picha 1: Washiriki wetu wameendelea kuhusika katika kuitegemeza kazi ya Bwana kwa njia ya matoleo.*

Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha kuwa si washiriki wote hushiriki katika utoaji wa zaka na sadaka, na baadhi ya wale wanaotoa hawatoi kwa ukamilifu kama ilivyoelekezwa katika maandiko. Hali hii inaathiri si tu maendeleo ya kazi ya Mungu, bali pia fursa ya washiriki hao kupokea baraka zilizoahidiwa kwa ajili yao.

## MALENGO 2022-2025

Malengo ya msingi ya Idara ya hazina katika kuhakikisha utume unaendelea vyema kwa kipindi hiki kinachomalizika ilikua ni pamoja na:

Kusimamia mapato na matumizi kwa kufuata mpango kazi wa mwaka uliopitishwa na Kamati Kuu, sambamba na kuzingatia miongozo ya fedha inayokubalika na Kanisa la Waadventista Wasabato Ulimwenguni.

Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani (Internal Control) ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji, na matumizi bora ya rasilimali za kanisa.

Kuhamasisha uaminifu miongoni mwa washiriki, kwa kutoa elimu ya zaka na sadaka.

Kuwajengea uwezo wahazini wa makanisa pamoja na watendakazi wengine katika kusimamia rasilimali za kanisa kwa mujibu wa kanuni, sera na miongozo ya kanisa.

Kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Conference.

Kusimamia, kuimarisha na kulea taasisi zetu – hasa za elimu na afya – ili ziweze kutoa huduma bora, kujitegemea kifedha, na kuchangia maendeleo ya kiroho na kijamii.

Kuboresha na kujenga nyumba za watumishi na wachungaji wa mitaa, kwa lengo la kuongeza ustawi wao na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Kulipa madeni ya ndani na yale ya taasisi, kwa kuzingatia mpango wa kifedha unaolenga kupunguza mzigo wa kifedha na kuimarisha uaminifu wa taasisi kwa wadau wake.

Kushiriki kikamilifu katika huduma ya Uinjilisti kupitia mpango wa Total Member Involvement (TMI), kwa kuhamasisha ushiriki wa kila mshiriki katika utume.

Kuendeleza watumishi wetu kielimu.

## VYANZO VIKUU VYA MAPATO YA CONFERENCE

Kwa mujibu wa ECD Working Policy (V14 na V25), vyanzo vikuu vya mapato ya Conference ni zaka na sadaka. Zaka hutengwa kwa ajili ya kuwahudumia wachungaji na watumishi wa kanisa, ili kuwawezesha kutekeleza kwa ufanisi kazi waliyoitiwa na Bwana. Aidha, sadaka hutumika katika kuendeleza kazi ya utume duniani, ikiwa ni pamoja na kufadhili miradi mbalimbali ya kanisa na maendeleo ya Conference kwa ujumla.




*Picha 2: Elder. Mwita Machage, Mhazini wa South Nyanza Field akiwasilisha somo juu ya umuhimu wa usimamizi wa fedha za Bwana katika semina iliyofanyika Mbela Misungwi.*


## MAPATO NA MATUMIZI

Tunamshukuru Mungu kwa wema na baraka zake kwa watu wake, pamoja na kuwawezesha kuwa waaminifu katika utoaji. Katika kipindi chote cha utendaji wetu, tumeshuhudia ukuaji wa mapato ya Conference, hususan kupitia Zaka na Sadaka.

Hata hivyo, licha ya ongezeko la washiriki, makanisa na mitaa, uwiano wa ongezeko hilo hauendani sawasawa na ukuaji wa mapato. Pamoja na changamoto hiyo, tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuendelea na kazi ya utume wa Kanisa lake.

| MAPATO (TSH) | MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2025- Agosti** | **2024** | **2023** | **2022** | **2021** |
| A. PATO LA ZAKA | | | | | |
| Jumla ya matoleo ya zaka | 3,468,934,371 | 5,912,115,238 | 4,956,057,642 | 4,575,984,446 | 3,915,548,460 |
| Toa iliyotumwa union | 1,117,396,027 | 1,998,365,218 | 1,711,408,192 | 1,524,442,380 | 1,290,192,022 |
| ***Jumla Zaka iliyobaki jimboni*** | ***2,351,538,344*** | ***3,913,750,020*** | ***3,244,649,450*** | ***3,051,542,065*** | ***2,625,356,438*** |
| | | | | | |
| B. PATO LA SADAKA YA PAMOJA | | | | | |
| Jumla ya matoleo ya sadaka | 1,276,766,679 | 2,142,075,554 | 1,738,228,640 | 1,646,002,883 | 1,395,360,529 |
| Toa iliyotumwa Union | 792,475,870 | 1,329,564,137 | 1,078,900,535 | 1,021,656,962 | 866,085,845 |
| ***Jumla Sadaka iliyobaki jimboni*** | ***484,290,809*** | ***812,511,417*** | ***659,328,105*** | ***624,345,921*** | ***529,274,683*** |
| | | | | | |
| C. MAPATO YA SADAKA ZINGINE | | | | | |
| Sadaka Zingine | 381,144,295 | 845,361,033 | 593,847,850 | 454,653,413 | 335,878,778 |
| | | | | | |
| ***JUMLA (A+B+C)*** | ***3,216,973,448*** | ***5,571,622,471*** | ***4,497,825,405*** | ***4,130,541,400*** | ***3,490,509,899*** |

*Jedwali 1: Mchanganuo wa Mapato kwa vipindi husika kuanzia 2021.*




*Kielelezo 2: Uwiano wa Matoleo katika kipindi cha kuanzia 2021 hadi 2025.*


## ULINGANIFU WA MAPATO YA ZAKA NA SADAKA

Ingawa kumekuwa na ongezeko la matoleo ya Zaka na Sadaka kadri miaka inavyosonga, bado kiwango cha Sadaka kimeendelea kubaki chini ikilinganishwa na Zaka.

Napenda kuwatia moyo waumini wote waendelee kumtolea Mungu kwa mpango maalum wa utoaji wa hiari ulio na utaratibu (Systematic Benevolence). Kwa kufanya hivyo, tutaendelea kuona uaminifu wa Mungu katika kutubariki, kama alivyoahidi katika neno Lake: *"Hata isiwepo nafasi ya kutosha"*.

| MATOLEO | MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2025- Agosti** | **2024** | **2023** | **2022** | **2021** |
| Zaka | 3,468,934,371 | 5,912,115,238 | 4,956,057,642 | 4,575,984,446 | 3,915,548,460 |
| Sadaka | 2,201,321,860 | 3,693,233,714 | 2,996,945,932 | 2,837,936,006 | 2,405,794,015 |
| ***Jumla*** | ***5,670,256,231*** | ***9,605,348,952*** | ***7,953,003,574*** | ***7,413,920,452*** | ***6,321,342,475*** |

*Jedwali 2: Ulinganifu wa matoleo ya Zaka na Sadaka kwa kipindi 2021 hadi 2025.*





*Kielelezo 3: Ulinganifu wa matoleo ya Zaka na Sadaka kwa kipindi 2021 hadi 2025.*

## UAMINIFU WETU KATIKA KIPIMO

Kwa sasa, Jimbo letu lina jumla ya washiriki 90,094. Hata hivyo, idadi ya waumini wanaoshiriki kikamilifu katika utoaji wa Zaka na Sadaka ni 18,018, ambayo ni sawa na asilimia 20 (20%) ya washiriki wote wa Jimbo letu.

Swali la kujiuliza ni hili: Je, ingekuwaje kama kila mshiriki angekuwa mwaminifu katika utoaji wa Zaka na Sadaka? Bila shaka, mapato ya Jimbo yangekuwa juu zaidi, na hivyo kuimarisha zaidi kazi ya utume na maendeleo ya huduma mbalimbali ndani ya Kanisa.

Ellen G White aliandika; "*Katika kazi hii malaika wote wa mbinguni wako tayari kushirikiana nasi. Rasilimali zote ziko chini ya wale wanaotafuta kuwaokoa waliopotea.*" Christ Object Lessons, uk. 197





*Kielelezo 4: Uwiano wa washiriki wanaohusika kikamilifu katika matoleo na wale wasiohusika.*

## MGAWANYO WA ZAKA NA SADAKA KWA NGAZI ZOTE ZA KANISA

| Zaka | Asilimia (%) |
|---|---|
| Zaka ya Zaka | 10.50% |
| Zaka Maalum | 15.00% |
| Mfuko wa Kustaafu | 12.50% |
| Msaada wa Elimu (Bursary) | 2.00% |
| TAMC | 2.50% |
| Heri Hospital | 1.00% |
| ECD Medical School | 1.00% |
| Pasiasi Hospital | 2.00% |
| Arusha University | 2.00% |
| Arusha Adventist College | 1.00% |
| Field/Field Mahalia | **50.50%** |
| ***Jumla*** | ***100.00%*** |

| Sadaka | Asilimia (%) |
|---|---|
| GC (General Field) | 20% |
| Division | 5% |
| Union | 5% |
| Field | 20% |
| Radio | 6% |
| Elimu | 2% |
| Kanisa Mahalia | 42% |
| ***Jumla*** | ***100.00%*** |

| Kambi | Asilimia (%) |
|---|---|
| Field/Field | 75.00% |
| Union | 25.00% |
| ***Jumla*** | ***100.00%*** |










## MATUMIZI

Kama taasisi, tunakabiliwa na gharama mbalimbali zinazohitajika kwa ajili ya uendeshaji wa kazi ya Mungu. Kwa kadri kazi inavyoendelea kukua, vivyo hivyo gharama za uendeshaji huongezeka.

Hali hii inatokana na uanzishaji wa mitaa mipya, ongezeko la idadi ya Wachungaji na watumishi wa kanisa, pamoja na fursa mpya zinazojitokeza kwa ajili ya kutekeleza kazi ya utume kwa ufanisi zaidi.

| MATUMIZI | MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2025- Agosti | 2024 | 2023 | 2022 | 2021 |
| Mishahara na Marupurupu | 1,975,840,374 | 3,370,800,747 | 2,907,967,080 | 2,741,663,426 | 2,406,655,176 |
| Matumizi ya ofisi | 534,428,496 | 1,482,599,221 | 1,368,985,579 | 1,284,075,285 | 1,124,794,576 |
| Uchakavu na samani | 79,963,049 | 198,430,062 | 167,849,928 | 92,854,897 | 111,620,602 |
| **JUMLA** | **2,590,231,920** | **5,051,830,029** | **4,444,802,587** | **4,118,593,608** | **3,643,070,354** |

*Jedwali 3: Muhtasari wa matumizi ya Jimbo katika kipindi chote cha taarifa hii.*





*Kielelezo 5: Muhtasari wa matumizi ya Jimbo katika kipindi chote cha taarifa hii.*

### *Baadhi ya Sababu ya Kupanda Kwa Matumizi*

1. Ukuaji wa Kazi ya Mungu
2. Ongezeko la Watumishi wa Kanisa
3. Ufunguzi wa Mitaa na Makanisa Mapya
4. Mahitaji ya Kitaaluma na Mafunzo Endelevu kwa watumishi wetu
5. Uboreshaji wa Miundombinu
6. Mabadiliko ya Kiuchumi na Gharama za Maisha (Mfumuko wa bei)

| Mwaka / Kipindi | Mfumuko wa Bei (%) |
|---|---|
| 2021 | 3.69 % |
| 2022 | 4.35 % |
| 2023 | 3.80 % |
| 2024 | 3.06 % |
| Mwisho 2024 / Jan 2025 | 3.1 % |
| Aprili 2025 | 3.2 % |




*Kielelezo 6: Mfumuko wa bei katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 (Chanzo. https://download.macrotrends.net/global-metrics/countries/TZA/tanzania/inflation-rate-cpi?utm)*

Washiriki wetu pia wameathiriwa na hali ya mfumuko wa bei inayolikumba taifa letu. Hali hii imepelekea baadhi yao kufikiria upya viwango vyao vya utoaji wa Zaka na Sadaka, wakihofia kutopata fedha za kutosha kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao binafsi ya kila siku.

Kwa sababu hiyo, kuna hatari ya kupata fedha kidogo kadri mfumuko wa bei unavyopanda, jambo ambalo linaweza kuathiri mapato ya Kanisa na utekelezaji wa kazi ya utume. Ni muhimu kuendelea kuelimisha na kuhamasisha waumini juu ya uaminifu katika kumtolea Mungu hata katika nyakati za changamoto za kiuchumi, kwa kuwa baraka zake ni za hakika wakati wote.

## HALI YA UJUMLA YA KIFEDHA

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, Conference yetu imeonyesha ustawi (muelekeo Chanya) wa kifedha unaosadifiwa na ukuaji wa rasilimali halisi za jimbo. Ukuaji huu unadhihirisha uimara na ustahimilivu wake, licha ya kukabiliwa na changamoto za kiuchumi zinazoathiri kwa kiasi kikubwa matarajio ya kiutendaji, hasa madeni yanayozikabili taasisi zinazomilikiwa na jimbo.

Ukuaji huu umejikita katika ongezeko la rasilimali, na kupungua kwa kiwango cha madeni tunayodaiwa. Hata hivyo, taasisi zilizo chini ya jimbo zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya kiuchumi, hali inayopelekea kuwa na kiasi kikubwa cha madeni ambayo yanalilazimu jimbo kuelekeza rasilimali zake katika kulipa madeni hayo, hivyo kuathiri ukwasi. Pamoja na hayo, tunamshukuru Mungu kwa uaminifu wake katika kubariki washiriki kupelekea ukuaji wa mapato ya jimbo, hivyo kuimarisha nafasi ya kifedha, kuboresha uwezo wa kutekeleza majukumu ya kifedha; ikiwemo ujenzi wa ofisi za jimbo, na kuongeza thamani ya jimbo.

Kwa ujumla mwenendo huu unaashiria kuwa jimbo letu liko katika hali nzuri ya kifedha, na tuko katika mazingira bora ya kustawi zaidi kwa siku zijazo. Jedwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa hali ya rasilimali za Jimbo katika kipindi chote cha taarifa hii.

| **A. RASILIMALI** | **2025-Agosti** | **2024** | **2023** | **2022** | **2021** |
|---|---|---|---|---|---|
| FEDHA TASLIMU NA BENKI | 224,981,068 | 256,910,478 | 369,398,218 | 84,155,724 | 134,906,210 |
| MADENI TUNAYODAI- Ruzuku ya madeni | 443,814,015 | 441,224,776 | 352,743,176 | 726,555,799 | 668,107,792 |
| VIFAA NA MALIPO YA AWALI | 212,781,274 | 149,178,318 | 166,740,963 | 121,714,182 | 52,989,504 |
| SAMANI | 1,354,598,284 | 1,673,759,132 | 1,397,717,129 | 1,094,872,965 | 907,347,362 |
| ***Jumla*** | ***2,236,174,642*** | ***2,521,072,703*** | ***2,286,599,486*** | ***2,027,298,671*** | ***1,763,350,869*** |
| | | | | | |
| **B. MADENI NA FEDHA ZA AMANA** | | | | | |
| MADENI TUNAYODAIWA | 238,080,664 | 515,980,367 | 745,917,594 | 390,326,887 | 377,385,214 |
| FEDHA ZA AMANA | 111,052,162 | 65,389,951 | 120,771,948 | 7,324,080 | 62,226,321 |
| ***Jumla*** | ***349,132,826*** | ***581,370,318*** | ***866,689,542*** | ***397,650,967*** | ***439,611,535*** |
| | | | | | |
| ***C. THAMANI HALISI YA JIMBO*** | ***1,887,041,816*** | ***1,939,702,385*** | ***1,419,909,944*** | ***1,629,647,703*** | ***1,323,739,334*** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| SDA Pasiansi Hospital | 465,851,240 | 439,055,108 | 196,881,504 | 210,572,147 | 198,222,208 |
| Nyanza Adventist High School | 206,741,520 | 205,776,774 | 183,164,892 | 290,878,018 | 281,601,385 |
| Bupandagila High School | - | 200,358,141 | 179,274,517 | 292,856,774 | 273,166,705 |
| Ngulyati Secondary School | - | 68,148,034 | 53,302,387 | 34,049,944 | 29,868,832 |
| Northern Tanzania Union | 158,087,686 | - | - | - | - |
| ***Jumla- Madeni ya Taasisi*** | ***830,680,446*** | ***913,338,056*** | ***612,623,300*** | ***828,356,883*** | ***782,859,130*** |
| ***MADENI YOTE*** | ***1,210,154,090*** | ***1,183,424,012*** | ***946,589,308*** | ***1,174,737,239*** | ***1,095,418,093*** |
| ***Uwiano wa madeni ya taasisi kwa madeni yote*** | ***69%*** | ***77%*** | ***65%*** | ***71%*** | ***71%*** |

## UJENZI WA MAKAO MAKUU

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa washiriki wote wa kanisa pamoja na wadau wa maendeleo kwa moyo wenu wa kujitolea katika kusaidia kazi ya Bwana. Tunathamini sana michango yenu ya mali, maarifa na ujuzi walioutoa kwa hiari katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa jengo la ofisi ya kazi ya Mungu South Nyanza Field unakamilika kwa mafanikio.

| Mwaka | Mapato | Matumizi | Salio |
|---|---|---|---|
| 2020 | 53,247,655.41 | - | 53,247,655.41 |
| 2021 | 15,446,427.08 | 4,100,000.00 | 64,594,082.49 |
| 2022 | 66,303,817.00 | 110,091,236.29 | 20,806,663.20 |
| 2023 | 302,785,682.26 | 243,160,143.00 | 80,432,202.46 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2024 | 236,412,317.95 | 299,986,652.43 | 16,857,867.98 |
| 2025 | 152,524,205.57 | 21,012,195.00 | 148,369,878.55 |
| ***Jumla Kuu*** | ***826,720,105.27*** | ***678,350,226.72*** | ***148,369,878.55*** |

**Salio la Jumla (Balance): Tsh 148,369,878.55**

## UJENZI WA NYUMBA ZA WACHUNGAJI

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa makanisa ya mitaa na wadau wote wa maendeleo ya kazi ya Mungu hapa South Nyanza Field kwa ushirikiano wao wa karibu na wa dhati. Kupitia ushirikiano kati ya washiriki, tumefanikisha ujenzi wa **nyumba 49** katika maeneo ya Mwanza na Simiyu; Ikiwa ni nyumba 15 Mwanza na nyumba 34 upande wa Simiyu. Pia tumeshirikiana na mtaa wa Kayenze kununua nyumba yenye thamani ya Milioni 30 Tzs (30,000,000). Jimbo limetumia kiasi cha 220,500,000 kusaidia ujenzi wa nyumba hizo.

Ujenzi wa nyumba za kanisa umekuwa na mchango mkubwa katika kupunguza gharama za upangishaji wa nyumba kwa watumishi wa Mungu. Zaidi ya kupunguza matumizi ya kifedha, nyumba hizi huchangia pia katika **kulinda heshima ya wachungaji wetu**, kwa kuwawezesha kuishi kwa utulivu bila bughudha kutoka kwa wamiliki wa nyumba za kupanga.

Tunaendelea kushukuru kwa jitihada za makanisa ya mitaa ambayo tayari ina viwanja na maboma yanayoendelea kujengwa, ikiwa ni pamoja na hatua mbalimbali za ukamilishaji wa nyumba za watumishi.

Tunatoa **wito wa dhati kwa mitaa yote ambayo bado haijaanza mipango ya ujenzi wa nyumba za watumishi**, kuanza mchakato huo mara moja. Ofisi ya Conference iko tayari kushirikiana na kutoa msaada kwa kadri inavyowezekana ili kufanikisha azma hii muhimu kwa ajili ya ustawi wa kazi ya Mungu.



## KUENDELEZA WATUMISHI WETU KITAALUMA

Tangu mwaka 2021 jimbo limefanikiwa kusomesha watumishi 27 wa kada mbalimbali kama ifuatavyo: - Meneja Miliki (1), Wachungaji (19), Secretary (1), Nesi (1), Waalimu (3), Wahasibu (2). Watumishi hawa wametumia kiasi cha **96,311,406.25** kufanikisha masomo yao.

## RUZUKU KWA TAASISI ZETU

Kwa dhamira ya kuendeleza kazi ya Mungu kupitia huduma za kijamii, **Jimbo limetoa ruzuku kwa taasisi zake za shule na hospitali**, Pamoja na vyombo vya Habari vya kanisa **(TAMC)** Ruzuku hii imelenga kusaidia maendeleo na uboreshaji wa huduma katika vituo hivyo muhimu, ili viendelee kutimiza majukumu yake kwa ufanisi na kwa viwango vinavyotarajiwa.

| ***Taasisi*** | ***Ruzuku ya Zaka*** | ***Ruzuku ya Sadaka*** | ***Jumla*** |
|---|---|---|---|
| Jiwekuu | | 7,000,000 | 7,000,000 |
| Pikipiki za Wachungaji | | 11,650,000 | 11,650,000 |
| SDA Pasiansi Hospital | 5,969,665 | 266,004,061 | 271,973,726 |
| Nyanza Adventist High School | | 210,673,030 | 210,673,030 |
| Bupandagila High School | | 159,692,970 | 159,692,970 |
| Bupandagila Primary School | | 33,706,875 | 33,706,875 |
| Ngulyati Secondary School | | 36,691,847 | 36,691,847 |
| NAVTC | | 88,482,705 | 88,482,705 |
| Vyombo vya Habari - TAMC | | 116,912,400 | 116,912,400 |
| ***Jumla*** | ***5,969,665*** | ***930,813,889*** | ***936,783,554*** |

## UTUME KWA MAENEO MAPYA (GLOBAL MISSION)

General Field, kwa kushirikiana na Jimbo letu, imeendesha miradi mbalimbali ya utume katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na huduma kikamilifu. Kupitia utekelezaji wa miradi hiyo, Jimbo limefanikiwa kufungua na kuanzisha mitaa mipya, ambayo ni matokeo ya kazi ya kimishenari iliyofanyika katika maeneo hayo. Mtaa wa Paji, Kayenze na Nyaruhande ni matokeo ya mradi huo. Kuanzia mwaka 2021 hadi sasa jimbo limetumia kasi cha shilingi **16,915,013.31**. Vilevile mradi umewezesha upatikanaji wa Pikipiki (7) saba kwa wachungaji wa Mitaa



## IDARA YA FEDHA NA UTUME

Kama idara, tumekuwa tukishirikiana kwa ukaribu na wahasibu wenzetu kutoka katika Unioni nzima katika kazi ya uinjilisti. Kila mwaka, tumefanya mahubiri ya pamoja, yanayolenga kuwafikia watu na kuimarisha imani ya washiriki, na ilipowezekana, kuanzisha na kujenga makanisa kama matokeo ya mahubiri yanayofanyika. Mwaka huu mwanzoni tulifanya Mahubiri kule Mara Field na kujenga Kanisa Eneo la Etaro. Mahubiri hayo yaliongoa watu 92.



## UKAGUZI NA FEDHA

Kanuni na miongozo ya Kanisa, kama ilivyoainishwa katika *ECD Working Policy*, inaelekeza fedha na mali za Kanisa katika kila ngazi na kila taasisi zitunzwe na kutumika kwa mujibu wa taratibu na miongozo rasmi ya utendaji wa Kanisa. Tunaamini kwamba utekelezaji mzuri wa matakwa haya unachangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha udhibiti wa ndani wa rasilimali, jambo ambalo huchangia pia kuongezeka kwa uaminifu miongoni mwa waumini na hatimaye kuongeza mapato ya Kanisa.

Katika kutekeleza lengo hili, tunafanya jitihada kuhakikisha kuwa Kitengo cha Ukaguzi katika Makao Makuu ya Conference (SNC) kinaimarishwa, na kwamba ukaguzi unafanyika kila mwaka katika kila kanisa la mtaa kwa kadiri inavyowezekana. Vilevile, tunafuatilia kwa karibu kuhakikisha kuwa taarifa za ukaguzi zinazotolewa na wakaguzi wa Conference zinafikishwa katika mabaraza husika ya makanisa na kuchukuliwa hatua stahiki kwa kujibu hoja zilizotolewa pamoja na kuweka udhibiti unaofaa ili makosa yasirudiwe. Utekelezaji wa hatua hizi umeleta ufanisi mkubwa, hasa katika makanisa ambayo yameonyesha ushirikiano kwa kupokea na kutii maelekezo ya jimbo. Kwa ujumla, tunashuhudia maboresho ya wazi katika taarifa za ukaguzi ndani ya Conference nzima. Tunawapongeza na kuwashukuru kwa dhati viongozi wa makanisa yote ambayo yanatekeleza mapendekezo ya ukaguzi kwa uaminifu.

Conference ya South Nyanza kama taasisi, imekaguliwa kila mwaka katika kipindi cha miaka minne mfululizo (2021, 2022, 2023 na 2024). Kwa neema ya Mungu, katika miaka yote hiyo, tumepokea hati safi za ukaguzi, jambo linaloashiria usimamizi bora wa fedha na mali za kazi ya Mungu.


Aidha, tumeona maendeleo chanya katika usimamizi wa fedha na mali katika taasisi zetu nyingine. Taasisi nyingi ambazo awali zilikuwa zikipewa hati chafu sasa zimeboresha utendaji wao; kwa sasa hatuna taasisi yenye hati chafu, bali chache tu zina hati ya mashaka, huku taasisi nyingine zikionesha mafanikio makubwa kwa kupata hati safi.

| Taasisi | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|
| **SNC Makao Makuu** | Hati Safi | Hati Safi | Hati Safi | Taarifa inasubiriwa |
| **Nyanza Adv Sec School** | Hati ya Mashaka | Hati ya Mashaka | Hati ya Mashaka | Haijakaguliwa |
| **Ngulyati Adv Sec School** | Hati Chafu | Hati ya Mashaka | Hati ya Mashaka | Taarifa inasubiriwa |
| **Bupandagila Adv Pri School** | N/A | Hati Chafu | Hati ya Mashaka | Haijakaguliwa |
| **Bupandagila Adv Sec School** | Hati Chafu | Hati ya Mashaka | Haijakaguliwa | Haijakaguliwa |
| **Pasiansi SDA Hospital** | Hati ya Mashaka | Hati Safi | Hati Safi | Hati Safi |

## UBUNIFU KWA AJILI YA UTUME

Katika kukabiliana na mabadiliko ya kasi ya teknolojia na mwenendo wa ulimwengu wa kisasa, Kanisa letu katika **South Nyanza Conference (SNC)** halijabaki nyuma. Kwa kushirikiana na **Kitengo cha TEHAMA**, **Idara ya Mawasiliano**, **Idara ya Uwakili**, pamoja na **Idara ya Hazina**, tumefanikisha uzinduzi na utekelezaji wa mfumo wa kidigitali wa shughuli za kanisa uitwao **Adventist Church Operations System (ACOS)**.

Mfumo huu wa kidigitali umeundwa mahsusi kwa ajili ya kurahisisha, kuharakisha na kuboresha usimamizi wa shughuli za kanisa kuanzia ngazi ya kanisa mahalia hadi jimbo. Aidha, umetatua changamoto nyingi zilizokuwepo awali, hasa katika maeneo yaliyokuwa yakitegemea kazi za mikono ya Mashemasi, Makarani, Wahazini, na Wachungaji.



*Faida na Majukumu ya Mfumo wa ACOS:*

1. **Kusajili washiriki** wa kanisa kwa usahihi na urahisi.
2. **Kukata risiti za matoleo** na kuchakata taarifa, huku mtoaji akipokea ujumbe wa kuthibitisha mchango wake.
3. **Kufanya hesabu za mgao wa asilimia ya matoleo** kati ya kanisa mahalia na ngazi ya jimbo.
4. **Kuandaa taarifa za mwisho wa mwezi**, zikiwa kamili na sahihi.
5. **Kuandaa "Jicho la Kanisa"** kwa ufuatiliaji wa mwenendo wa kifedha.
6. **Kuchambua mwenendo wa matoleo**, kwa kila kanisa mahalia na jimbo kwa ujumla.
7. **Kuandaa taarifa za matoleo ya mshiriki** kwa kila mwezi hadi mwaka (Member Statement).
8. **Kutekeleza majukumu mengine muhimu**, ambayo bado yanaendelea kuboreshwa na timu ya TEHAMA.

Kupitia mfumo huu, tumepunguza kwa kiwango kikubwa matumizi ya karatasi (paperwork), na hivyo kuleta ufanisi mkubwa katika utendaji wa kila siku wa kanisa.




*Matarajio Yetu*

Tunatarajia kuendelea **kuimarisha Kitengo cha TEHAMA**, kwa lengo la kuhakikisha kuwa kanisa katika ngazi zote za jimbo linaendelea kufanya kazi kwa weledi na kuendana na maendeleo ya kiteknolojia ya sasa. Tunaamini kuwa hatua

hii ni muhimu katika kulifanya kanisa kuwa la kisasa, lenye ufanisi, na linalotoa huduma bora kwa washiriki wake.

Ili kupunguza matumizi ofisi yetu pia inaendelea na majaribio ya bahasha maalum yenye uwezo wa kutumika kwa Zaidi ya miezi sita hadi Mwaka.

## MIPANGO 2026-2030

1. Kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa Mujibu wa Mpango Kazi wa 2026-2030
2. Usimamizi Madhubuti wa Mapato na Matumizi ya jimbo
3. Kuimarisha Mfumo wa Udhibiti wa Ndani (Internal Control) kwa ngazi ya jimbo na makanisa mahalia
4. Kuhamasisha Uaminifu kwa Waumini kwa ushirikiano na Idara ya uwakili
5. Kukuza na kueneza uelewa juu ya njia bora za usimamizi wa rasilimali za Mungu
6. Kukamilisha Ujenzi wa Ofisi Kuu ya South Nyanza Conference
7. Usimamizi na Uboreshaji wa Taasisi za Elimu na Afya
8. Kuboresha Miundombinu ya Makazi ya Watumishi
9. Kuimarisha uwezo wa kujitegemea kiuchumi na kukuza ukwasi.
10. Kuhusika Kikamilifu katika Huduma ya Uinjilisti (TMI – Total Member Involvement)
11. Kuunga mkono mipango kazi ya Idara zote katika kufanikisha utume
12. Kuongeza ubunifu wa kazi, Zaidi katika Teknolojia
13. Kuwaendeleza watumishi wetu kielimu
14. Kushirikiana na idara ya Elimu kuanzisha Shule ya Msingi Jijini Mwanza.
15. Kuongeza mitaa yote kwenye mfumo wa ACOS

## KUJIANDAA NA MATUKIO YAJAYO

Hali ya ulimwengu leo ni onyo la changamoto kubwa zaidi zinazoweza kujitokeza siku zijazo. Hali hii imefungua fursa ya kuchunguza njia mpya za kufikiri na kutekeleza utume, ikiwa tutachukua muda wa kutafakari na kuomba kwa bidii.

Kanisa (na taasisi zake) linapaswa kujenga uwezo wa kustahimili hali ngumu ya kiuchumi, ambayo inaweza kuhatarisha rasilimali muhimu kwa ajili ya kazi ya Mungu. Kupanda kwa bei za chakula, nishati, na mfumuko wa bei kwa ujumla kunaleta changamoto kubwa kwa maisha ya kila siku.

Katika mazingira haya, tunaitwa kutumia rasilimali zetu kwa hekima, kama alama ya uaminifu kwa Mungu. Licha ya changamoto hizi, tunaelewa kuwa tunaelekea ukingoni mwa historia ya dunia hii. Kama alivyoandika Ellen G. White:

“Maafa ya nchi kavu na baharini, hali isiyotulia ya jamii, kengele za vita… vinatabiri matukio makubwa yanayokaribia. Mabadiliko makubwa yatatokea hivi karibuni katika ulimwengu wetu, na harakati za mwisho zitakuwa za haraka.” *(White, 1909. Mashauri kwa Kanisa, Gombo la 9 – tafsiri isiyo rasmi)*

Ni wakati wa kufanya kazi ya Mungu kuwa **uwekezaji wetu mkuu**. Tuitumie mali zetu sasa kwa ajili ya kazi yake, kabla hazijapoteza thamani na kutokuwa na faida kwa utume

Idara ya fedha inafanya kazi kwa ukaribu sana na idara ya uwakili. Na katika ubia huu tunatamani washiriki wote wajue wajibu wao kwa Mungu, nasi tunaongozwa na Imani hizi:-

1. Tunaamini kwamba uwakili wa mali ni kuhusu kukuza Imani za washiriki wetu, si kuongeza wingi wa fedha.
2. Tunathamini uaminifu na imani ya washiriki wa kanisa kwetu.
3. Tunaamini kwamba kanuni za uwakili wa mali huongoza kila nyanja ya maisha yetu ya kila siku.
4. Tunatarajia kuwa washiriki wa kanisa watakua katika uhusiano wa kina na Mungu.
5. Tunaamini kwamba usimamizi bora wa mali ni kwa ajili ya kila mtu, kila mahali, na kila wakati.

## HITIMISHO

"Siri ya mafanikio yetu katika kazi ya Mungu itapatikana katika ushirikiano wa watu wetu wanaofanya kazi kwa umoja. Lazima kuwe na juhudi za pamoja. Kila mshiriki, kama kiungo cha mwili wa Kristo, hana budi kutimiza wajibu wake katika kazi ya Mungu; kulingana na uwezo aliopewa na Mungu. Tunapaswa kushirikiana kwa karibu na kushikamana kwa umoja wa kikristo katika kukabiliana na vikwazo na changamoto — bega kwa bega, kwa kutiana moyo."

*Review and Herald*, December 2, 1890